HALMASHAURI YA WILAYA PANGANI

TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO YA TATU JANUARI HADI MACHI, 2018

UTANGULIZI
Mh Mwenyekiti

Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Halmashauri imepanga kutekeleza bajeti yake yenye jumla ya **Shilingi 14,515,222,926/-** zinazotarajiwa kukusanywa katika vyanzo mbalimbali ikiwemo makusanyo ya ndani, ruzuku kutoka serikali kuu pamoja na ruzuku kwa ajili ya miradi ya maendeleo kutoka kwa wahisani.

Kiasi hicho cha fedha pia kimepangwa kutumika kugharamia matumizi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kulipa mishahara ya watumishi, kugharamia miradi ya maendeleo katika maeneo yote ya wilaya ya Pangani na matumizi mengineyo.

1. MAPATO
Mh Mwenyekiti

Hadi kufikia robo ya tatu Januari - Machi 2018, Halmashauri imeweza kukusanya jumla ya shilingi **8,884,489,596/-** sawa na asilimia **61** ya makisio ya mwaka kutoka kwenye vyanzo mbalimbali kama jedwali namba 1 linavyoonyesha hapa chini.

Jedwali Na. 1: Mapato robo ya tatu Januari - Machi, 2018

Na	CHANZO CHA MAPATO	MAKISIO MWAKA 2017/2018	JUMLA YA MAPATO JULAI HADI DESEMBA, 2017	JUMLA YA MAPATO JANUARI HADI MACHI, 2018	JUMLA YA MAPATO JULAI 2017 HADI MACHI, 2018	MAPATO PUNGUFU/ZAIDI	ASILIMIA
1	Mapato ya ndani	1,290,012,426	500,721,726	251,847,029	752,568,755	(537,443,671)	58
2	Mishahara	9,736,902,500	3,977,736,000	2,014,229,215	5,991,965,215	(3,744,937,285)	62
3	Mapato ya ruzuku ya matumizi ya kawaida	632,816,000	257,038,800	45,674,000	302,982,800	(329,833,200)	48
4	Mapato ya ruzuku ya miradi	2,855,492,000	1,263,493,866	573,478,960	1,836,972,826	(1,018,519,174)	64
	JUMLA	**14,515,222,926**	**5,999,260,392**	**2,885,229,203**	**8,884,489,596**	**(5,630,733,330)**	**61**

2. MATUMIZI

Mh Mwenyekiti,

Katika kipindi cha kufikia mwezi Desemba, 2017, jumla ya Shilingi **5,104,456,237.91/=** zimetumika na kufanya matumizi kufikia asilimia **35** ya makisio ya mwaka, na zimetumika katika vyanzo mbalimbali kama jedwali namba 2 linavyoonyesha hapa chini.

Jedwali Na. 2: Matumizi hadi Desemba, 2017

NA	CHANZO CHA MATUMIZI	MAKISIO MWAKA 2017/2018	JUMLA YA MATUMIZI JULAI HADI SEPTEMBA, 2017	JUMLA YA MATUMIZI OKTOBA HADI DESEMBA, 2017	JUMLA YA MATUMIZI JULAI HADI DESEMBA, 2017	MATUMIZI PUNGUFU/ZAIDI	ASILIMIA
1	Mapato ya ndani	1,290,012,426	119,740,731`	293,154,857	412,895,588	877,116,837	32
2	Mishahara	9,736,902,500	2,001,499,000	1,977,856,000	3,979,355,000	5,757,547,500	41
3	Mapato ya ruzuku ya kawaida	743,696,965	72,289,524	136,137,584	208,427,108	535,269,856	40
4	Mapato ya ruzuku ya miradi	2,706,230,013	182,798,683	320,979,857	503,778,540	2,202,451,472	28
	JUMLA	**14,476,841,904**	**2,376,327,938**	**2,728,128,300**	**5,104,456,238**	**9,372,385,666**	**35**

MAFANIKIO

Mh Mwenyekiti,

Makusanyo ya vyanzo vya ndani pekee ni jumla ya **Shilingi 752,568,755/=** sawa na **asilimia 58**. Mapato haya yamechangiwa na baadhi ya vyanzo vya mapato kufanya vizuri kwa zaidi ya asilimia **75** iliyopaswa kufikiwa mwezi Machi, 2018 kwa lengo la kiasi cha **Shilingi 967,509,320/-** Vyanzo hivyo ni kama ifuatavyo:-

- Leseni za biashara Sh. 32,530,786/- sawa na asilimia 93
- Ada ya ukaguzi wa wanyama Sh. 2,776,750/- sawa na asilimia 93
- Ada ya Machijio ya wanyama Sh. 2,438,360/ - sawa na asilimia 98
- Ushuru wa mazao ya bahari Sh. 142,272,805/- sawa na asilimia 97
- Ada ya kuegesha magari stendi Sh. 12,689,750/- sawa na asilimia 76
- NHIF/NSSF Sh. 346,347,877/- sawa na asilimia 94

CHANGAMOTO

Mh Mwenyekiti

- ✓ Upungufu wa vifaa vya kukusanyia mapato na kuharibika kwa vifaa hivyo mara kwa mara.
- ✓ Kutozingatiwa kwa sheria ndogondogo katika ukusanyaji wa mapato ya ndani kunapelekea kupungua kwa mapato.
- ✓ Kuwepo kwa mgogoro katika eneo la soko na stendi juu ya kodi ya vibanda ambayo hailipwi kwa usahihi.
- ✓ Baadhi ya sheria ndogo kutokidhi haja ya wakati wa sasa katika ukusanyaji.
- ✓ Kushuka kwa morali ya wakusanyaji kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo motisha.
- ✓ Baadhi ya vyanzo vyenye bajeti kubwa kurudishwa serikali kuu kumepelekea kupungua kwa mapato.Mfano kodi ya majengo, kodi za mabango (ada ya matangazo) na Kodi ya ardhi 30%.

MIKAKATI

Mh mwenyekiti

- ➢ Tunategemea kuanzia mwezi April, 2018 kutawasili POS mpya kwa ajili ya kuwapatia watendaji wa vijiji walioajiriwa hivi karibuni ili kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato.
- ➢ Kufanya ufuatiliaji wa sheria ndogo zilizotungwa hivi karibuni.
- ➢ Kuboresha sheria ndogo kila panapohitajika kufanya hivyo ili ziendane na wakati.
- ➢ Kutazama upya namna ya makusanyo yanayokusanywa na wakusanyaji wetu ili ukusanyaji wao uwe na tija kwa pande zote mbili.
- ➢ Kuhakikisha vile vyanzo vilivyobaki kwetu Halmashauri vinasimamiwa kikamilifu kuanzia ngazi ya kijiji, kata na wilaya kwa kushirikiana kuziba mianya ya upotevu wa mapato ili tuweze kufikia lengo.

Mchanganuo wa mapato yote na matumizi ya Halmashauri umeonyeshwa kwenye majedwali yaliyoambatanishwa na taarifa hii.

Naomba kuwasilisha.

.....
DAUDI O MLAHAGWA
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
PANGANI